

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

VERBATIM REPORT OF

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,

KASARANI CONSTITUENCY,

AT MATHARE NORTH SOCIAL HALL

ON

WEDNESDAY, 29TH MAY, 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, KASARANI CONSTITUENCY, HELD AT MATHARE NORTH
SOCIAL HALL, ON WEDNESDAY, 29TH MAY, 2002**

Present

1. Com. Idha Salim
2. Com. Kavetsa Adagala

Secretariat in Attendance

1. Samuel Wanjohi - Programme Officer
2. Esther Mugo - Asst. Programme Officer
3. Martina Odhiambo - Verbatim Reporter

Meeting started at 9.00 a.m. with Com. Salim in the Chair.

Mr. Wanjohi: Tutaanzisha kikao, lakini tutamtumania Com. Kavetsa Adagala atafika wakati wowote na tungetaka kumuuliza huyu kijana ndugu yetu atuanzie kikao chetu kwa maombi, wengine watatukuta tukiendelea. Kuja.

Speaker: Thank you so much. Let us all stand for a word of prayer. Our heavenly Father, we want to thank you this wonderful morning that you have given to us. Lord, as we are gathering here for this wonderful session in the history of our Country, we want to ask Lord that you give us the wisdom to participate in this noble course. We want to pray for our brothers and sisters who are still on their way coming here that you be their guidance and protector, in thy mercy keep them safe, Lord bring them here so that they may participate together with us. We want to put all the Commissioners in thy might hand Lord, let them realize that the work they are doing for the Country is of a noble course and let them Lord, give them strength to pursue and to achieve all the goals that they have set. Thank you Father for everything. I commit this day in thy

might hand. Whatever will take place today, Lord, be the guider and protector. Above all Lord, protect each and every soul that will be presented here. In the mighty name of Jesus Christ I pray and believe. AMEN.

Mr. Wanjohi: Thank you. On behalf of the District Co-ordinator-- Maina atakuja, Professor, baadaye, ameanza huko upande ya Embakasi, lakini atakuja hapa baadaye. Ningetaka kuwajulisha wale members wa committee yetu ya Constituency waliofika, pengine wasalimie watu kidogo because I don't know them Mheshimiwa Muchiri na yule mzee mwingine. Tuna wangapi? Mheshimiwa, salimia watu just before we start na huyo mwingine member wa committee, kuja salimia watu pia and tell them your name. Do we have another one? Mheshimiwa ni member wa committee yenu ya Constituency, nilikuwa na yeye jana, nafikiri Commissioner tutamshukuru kwa sababu ametusaidia. Salimia watu.

Mhe. Muchiri: Mr. Chairman, thank you very much for your coming here. I wish to inform you that the Public has been informed. Even this morning, I met a young man who was advertising. We have also tried our level best to advocate about the Constitutional Review. Now, the other thing is that, Mr. Chairman, we are grateful that you are always punctual at your work. Thank you.

Mr. Wanjohi: Thank you Mheshimiwa Muchiri. You have been with us since yesterday. Asante sana pia.

Daniel Peter Mbeka: Good morning all of your? Now, on behalf of the 3 Cs, my name is Mbeka Daniel Peter. I wish to welcome the Commissioners to this place – Mathare which is a part of Kasarani. This house will be full according to the work which we did because I have not seen people from as far as Baba Dogo, they are still coming, the far end of Kasarani, they are still coming which means Kariobangi is not yet here, Korogocho is not yet here. So, be peaceful and I know that we will a nice work today and we look towards the change which is going to be in the Constitution. Otherwise, thank you. Feel welcome, thank you.

Com. Salim: Thank you very much everybody, good morning. I am very happy to be here. My name is Ahmed Idha Salim. I am a Commissioner, I am also one of the Vice-Chairpersons of the Commission. I want to thank the Members of the Committee. Mheshimiwa Bwana Muchiri and his colleague who has just come up to introduce themselves for the work they have done not only today but for quite a number of weeks now, preparing the people for this very very important meeting and we are sure that this place will probably be more than full. It is our experience that everywhere we go, it takes time for Wananchi to attend such meetings. There are the lots of other commitments, a lot of other things to attend to first thing in the morning, so we know, it takes time to finalise other very important matters before coming to this important meeting like this one. So, we are convinced that we will a lot of people coming to give their views today.

Let me introduce other members of staff here, who are helping us collect views. I have, of course the Programme Officer – Bwana Samuel Wanjohi there, very hard working Programme Officer at the Commission who is in charge of making sure that everything goes well for this meeting.

And over there, we have Millicent whose job is equally very very important. She is the translator – is sign language expert. In case any one of us has difficult hearing or cannot hear at all, she can help translate what is being said to that person and vice versa. Get us his views, he does not have to speak using sign language, he can also give his views. So, she is there to this very important job.

And over there are two ladies. We have Martina Odhiambo over there. She has an important task of noting down your views – verbatim, word for word. Ana experience kwa jambo hilo. And then next to her is a young law student of ours, also helping to do the same thing and, is it Esther? Esther yes.

And other than that, we are expecting my colleague – Com. Kavetsa Adagala. She is held up on some other matter concerning the Constitution somewhere but will be joining us very soon. But because we anticipate a large number of people coming this morning to give their views, we can start and then she joins us so that we don't hold up people for too long. As soon as the register, we would like to get their views.

We can collect views in two ways. Wananchi can either (aah I am very pleased, my colleague Com. Adagala as I told you will be here any minute and she is walking in now. Karibu sana Kavetsa. Com. Adagala is a lady of many parts. She has been involved in such national functions as the music festival, she is a senior lecturer of many years standing at the University of Nairobi and I am very happy to have her here in this very important day of collecting views).

As I was saying, wanachi can give views in two ways. Either, they can come up and just present their views orally or they can present their views through a memorandum (written views). Now, for those who want to present views orally, we give them five to six minutes because we don't know how many Wananchi will be coming to give their views and we want to be sure that they all get a chance. So, we have to limit the amount of time unfortunately each mwanachi can take to give his views. At least for the time being and see how things move in the course of the day. Those who have views already written (tayari kabisa) will be given two-three minutes not to read their memorandum, but to highlight, give the recommendations or the proposals they want to give for the review of the Constitution or changes in the Constitution. So, let us all stick to that arrangement, but of course we do understand that there is need for clarification, my colleague or I need something explained, it means mwananchi will take longer to complete the work of giving his views. So, those are the two ways we will be collecting views. Views can be given in any language – can be Kiswahili, the national language, can be in English, the official language, can be in any local Kenyan language – Kikuyu, Kiluo, hopefully there will someone in the audience who can translate for us if any mwananchi cannot or does not want to speak English or Kiswahili. We should only remember one thing, if you do can

Speak English or Kiswahili, please use it, only for one reason, it will save time. If we have anything translated from any other language, we double the time. Mwananchi will speak in one local language but then we will have to translate the whole thing again in Kiswahili for recording purposes. So, I hope we all appreciate this arrangement and we can therefore now start unless my colleague wants to say Jambo to everybody before we start.

Com. Adagala: Habari za asubuhi watu wa Mathare? Tumefurahi sana kufika hapa na ninafikiri tutaendelea vizuri. Mathare ina watu wengi na nitataka watu wengi watoe maoni yao vile wanaona Kenya mpya inaweza kukaa. Sasa sina mengi ya kusema, nimefurahi kuwa hapa. Asante.

Com. Salim: Asante Com. Adagala. Let me now call then the first person who has registered. This is how we will be following the programme – first come, first served. So, we would like to ask Bwana Simon Karanja. Simon Karanja kuja kutoa maoni yake. Yeye atatoa maoni nafikiri ki-mdomo.

Simon Karanja: Jina langu ni Simon Karanja. Maoni yangu iko kwa upande wa mashamba. Kuna mashamba, watu wako na mashamba ambayo hawaitumii na kuna watu wengi, wengine ambao hawana mahala pa kukaa. Kwa hivyo hayo mashamba yagawiwe watu ambao hawana hata mahali pa kuzikwa sababu kuna watu wengine wanazikwa kwa City Council. Ningependelea, hayo mashamba yagawiwe watu ambao mahali popote. Serikali igawie hao watu ambao hawana mashamba maana haya mashamba yako chini ya serikali. Kwa hivo hayo mashamba yagawiwe watu ambao katika Jamhuri ni wa serikali. Nimemaliza, yangu ilikuwa ni hiyo tu.

Com. Salim: Asante sana Bwana Simon Karanja kwa maoni yako mafupi na ni lakini wazi kabisa ni kuhusu mashamba. Asante sana. Elias Njoroge.

Elias Njoroge: Hamjambo, hamjambo Wananchi? Maoni ni

Com. Adagala: Njoroge! Hapa, ni Tume pekee hiko hapa. Ukizungumza, unazungumzia Tume, okay!

Elias Njoroge: Maoni yangu, ningependa, uwezo wa Rais upunguzwe. Na upande wa mahakama, ipewe uwezo wake. Na kuwe na Prime Minister. Na tena kama upande wa Polisi, Polisi wapewe uwezo wa kufanya kazi. Yaani kama Mkubwa wa Polisi, awe akiteua maofisa wake.

Com. Adagala: Nani atachagua Mkuu wa Polisi?

Elias Njoroge: Nimefahamu. Tena, upande wa mashamba, kuwe na mtu ambaye anasimamia mashamba kugawa.

Com. Salim: Kugawa, kumpa nani? Na ni nani huyo ambaye atagawa?

Elias Njoroge: Mtu ateuliwe na serikali. Maoni yangu ni hayo.

Com. Salim: Agawe mashamba gani?

Elias Njoroge: Yale ambaye imenyakuliwa na watu binafsi.

Com. Adagala: Asante. Ugependa mashamba ile imenyakuliwa.

Elias Njoroge: Igawiwe Wananchi wale hawana mashamba kwa sababu kuna Wananchi wengi hawana mashamba, hawana pahali hata pa kukaa.

Com. Adagala: Okay, twende nyuma mpaka mwaka gani kwa wale walinyakua. Unajua wengine wanasema 1990, wengine wanasema 1980, wengine wanasema 1963.

Elias Njoroge: 1960

Com. Adagala: Halafu unaona mtu ambaye hana shamba au watu hawana shamba, wapate kiasi gani ya shamba?

Elias Njoroge: Hata kama ni acre mbili ama tatu

Com. Adagala: Acre tatu hivi?

Elias Njoroge: Eeh.

Com. Adagala: Na shamba kubwa lenyewe liwe gani, acre ngapi? Watu wamenyakua, wana mashamba maelfu ya acre, na watachukuliwa. Lazima ifike kiwango fulani. Ya juu sana iwe acre ngapi?

Elias Njoroge: Hata kama iwe ni acre tano.

Com. Adagala: Ya juu sana?

Elias Njoroge: Eeh.

Com. Adagala: Okay.

Com. Salim: Asante sana Bwana Elias Njoroge. Bwana Odera Ondiege.

Odera Ondiege: I prefer so much to speak in English. My first contribution is about a majimbo system of government. I so much recommend majimbo system of government because for one thing, it will be divided on the region basis. The region basis as per my thinking should be the Provincial Administration boundaries where in Kenya we should have eight regions or eight jimbo. My recommendation for this follows:-

1. Each Province in the Republic of Kenya is gifted, can produce excess of a particular item against the other region. For example, Nyanza Province. In Nyanza Province, there is a lot of sugar cane growing, there is rice at Kano and again if you come to Rift Valley, there is a lot of tea being grown but is not in Nyanza. So, with this, the people of Rift Valley will be allowed to plant a lot of tea while the people of Nyanza will be allowed to plant and harvest a lot of sugar and in the interim, they will be allowed to exchange. The money so collected, will be planted back in the same region except a small fraction will be forwarded to the Central Government to run the economy of the country as tax.

This kind of competition will encourage other regions to compete against the best because the people of Nyanza will say, if we are lagging behind and the people of Rift Valley have gone so much, let us follow them very speedy and at the end of it all, the whole country will develop economically.

What again I would like to add is this, each Jimbo should be given some degree of autonomy where the torch-bearer of that region can source for funds and development projects outside the country and this one will bring what we call development jealousy. The development jealousy is another region that has not got strong torch-bearer to source for development projects abroad will also come up and say, we also have to go abroad or anywhere else and source for this development. So, within the competitions, we will come up and develop the whole nation unlike what it is now where everything is centralised at the government, every region is sitting back waiting for the government to do. So, to us all, we are saying, this is the work of the government and at the end of it all, every region is lagging behind in all aspects.

2. I would like to talk about affirmative action. I personally reject the affirmative action because this is a kind of a discrimination. Affirmative action as our fellow women/ladies are asking for it. For example in politics, they are suggesting that out of 210 Constituencies, a good fraction be set aside for them where men don't compete for such Parliamentary seats or civic seats. What I am saying is this, I recommend that all these elective posts be very competitive so that we get the best. We have no time to say women are rejected from these areas or men are rejected from these areas or certain people with certain disabilities are rejected from this area, No! Everybody should be given equal chance to compete and from this angle, we will get the best.

3. Semi-Defections. Semi-Defections is a case where somebody sits in a Party and declare interest for another Party while he sits on this one. The next one is education of candidates.

Com. Salim: Do not explain, we already understood. What should the law say about them?

Odera Ondiege: The law should say, if you are in a particular Party, sit and stick there. Another point is about education of candidates. We should have at least education of all candidates because this is a case where you find an M.P. on a Budget Day, the Minister of Finance is reading the Budget and M.P.s are just sleeping because they don't understand what is going on.

Another point, number of Political Parties. Number of Political Parties should be regulated upto a certain angle I am going to say. We have got over 40 registered Political Parties. My proposal, any registered Political Party after general elections that fails to win any Parliamentary seat should automatically be deregistered.

I would have like also to talk about land re-distribution. In my point on land re-distribution, it is very shameful on us Kenyans where a Politician owns three plots. My proposal is, no one should have more that five plots in an urban centre. Unless there is a specific question, I feel to end there.

Com. Adagala: I can have five plots in Nakuru, five in Nairobi, five in Mombasa, is that what you mean?

Odera Ondiege: Five in total in the whole Republic of Kenya urban centres.

Com. Salim: Okay. On same point, the plots can be any size? Can be ten acres, twenty acres, hundred acres multiply by five?

Odera Ondiege: If it is in acres, then it ceases to be a plot. That is now land.

Com. Salim: But a plot is a plot?

Odera Ondiege: Especially where we are staying here, any structure is a plot.

Com. Salim: But my friend you know you have to look beyond this area and also beyond this year, beyond this decade. We are writing a Constitution for hopefully 200-300 years. So we really have to see far. So, what would you like to see?

Odera Ondiege: Exactly. The more we are living, the more people we have. So, what I mean by a plot is '80x40'

Com. Salim: There you are, that is much better, more specific. Thank you.

Odera Ondiege: Thank you also.

Com. Salim: Bwana Mheshimiwa. Bwana Muchiri, karibu.

Mhe. Muchiri: Mr. Chairman, you remember yesterday, I contributed a lot but I forgot three points. One, there should be a clause concerning the NGOs that when they come to operate in particular Constituencies or Areas, the residents of that Area should be consulted on what they are doing and there must be agreement on the process they will take within that Constituency.

Two, probably, there should be a clause in the Constitution to protect public utilities.

Three, the Speaker of National Assembly should be elected by the public not by the Members of Parliament.

Four, the Constitutional Review is a process that will continue for a long time. It should not be based on the time-table that is given. It should be entrenched in the Constitution and be made a process that will continue as we normally have the process of the registration of Identity Cards.

Five, there should be a clause indicating the freedom of worship. We have so many religions protruding within the country. Some we don't know, what, how they process their teaching like devil-worshippers. There should be a clause to indicate what the teachings they follow.

The last one, Mr. Speaker, yesterday, I talked about the issue of the youth being arrested by the Police. Once a Policeman has arrested someone, there should be a clause in the Constitution that the person arrested must be informed in writing immediately he arrives at the Police Station indicating the offences he has been charged for. Currently, the Police are arresting the youth, taking them to the Police Station and eventually when they lack the offences to charge them, they are fabricating cases within the Police Station. That is what I had. Thank you.

Com. Salim: Thank you very much Mheshimwa. Good to talk to you again. Hold on a minute. This question of worship, I don't know what we shall do about it because, it can easily turn into witch-hunting because it is not clear what devil-worship is and so it may be, I can see, a Muslim can decide he is a devil-worshipper. He can see me as a devil-worshipper or we can see someone else both of us as a devil-worshipper. So, I don't know what the parameter is or what the indications are for devil-worship? Because you are saying there is a clause, so that clause would have to say what is rightful worship and what is wrongful worship. So, you would have to tell what that wrongful worship is.

Mhe. Muchiri: You see the problem we have today is that nobody understands upto what level the freedom of worship is. You can put a cow there, you can put a goat, you can put a spear and his speaker and you start worshipping it. The issue has now cropped out that we have got so many religions, we have got about 800 registered religions in this country. They all preach about Jesus and about the Muslim Community and the Hinduism and the rest. But, at the centre, there is nobody, nobody, no institutions that investigate about the worshipping. Even the amount they collect of money in this country, they don't even account for it. There should be a clause indicating exactly what they do after they preach and what they do with the account of the money that they collect from the public.

Com. Salim: Asante sana Mheshimiwa. That is much clearer now. We call now Lawi Ogila. Lawi Ogila yuko? Excuse me Bwana Ogila, keep it when you finish, you hand it over there.

Lawi Ogila: Thank you. I have three areas to discuss. They are further discussed in the memorandum which I will be giving but I am going to talk on one of the issues which I feel the Constitution of Kenya should be addressing.

The issue is political assassinations, and I will be reading. The issue of political assassination must be fully explored in the Constitution for Kenya to really move forward. This delicate yet important area of decision, discussion must be constitutionally addressed and proper conditions put in place to avoid this dark side of Kenya's life style.

Com. Salim: Excuse me Mr. Lawi, it would not be possible for you to read. You will give us your proposal, not your description. A one sentence proposal on everything that you have said. We shall read the memoranda. We shall sit down and read the memorandums, all of them.

Lawi Ogila: Okay, thank you.

Com. Salim: What do you want to say about political assassinations?

Lawi Ogila: Everything to do with all the political assassinations will be addressed in the memorandum. Thank you.

Com. Salim: Excuse me, what is your one sentence on political assassination because we have put it down already, so we want to know what you want to say about it.

Lawi Ogila: I want the Government of Kenya and the people of Kenya to make sure that political assassinations or what has been termed as political assassinations must be fully given public hearing and the findings must be made public. I have finished, thank you.

Com. Salim: Your only point is on political assassinations?

Lawi Ogila: I said, I had three areas to present

Com. Salim: Give us your second one then.

Lawi Ogila: Well, first of all, Christian approach, I think the Constitution should allow Kenyans to have the freedom of worship. Also, human rights approach, I would like the issue like it happened recently where Abdul Ochan was arrested in Kenya. I want the Constitution to address such issues so that our Kenyan status of human rights can conform to the international standards of other countries.

Com. Salim: Is that all Bwana Lawi?

Lawi Ogila: Yes.

Com. Salim: You said you had about four points. We have noted three. Have you finished with all of them now?

Lawi Ogila: Sorry, I said I had three but I was going the last one which was political assassination, which was due to because of time, but I have them in writing.

Com. Salim: Thank you. Thank you very much Bwana Lawi. As my colleague told you, we will take your memorandum and read it. All memoranda will take and read very carefull by the Commission. All we need from people presenting memoranda is that they should just highlight the points in their memoranda. Thank you very much for your views. We move on to

Com. Adagala: Mr. Lawi, hallow, Mr. Lawi. You are aware that a freedom fighter can be a terrorist and a terrorist can be a freedom fighter. So, international standards become a problem because when you present that point, you must say that Kenya must state its stand, okay. You need to state the stand on human rights on that particular point. Okay, thank you.

Com. Salim: Henry Mosei. Ooh, he is a listener, okay. Gerald Ochieng – listener, umekuja kusikiza tu nafikiri? E. M. Mong'are, karibu.

Com. Adagala: District Co-ordinator, is the District Co-ordinator here? Okay. Are the Committee Members here?

Response: Yes.

Com. Adagala: We want to see women participating and disabled and.... well, here everybody is mixed but we really hope you have mobilized because now we see only one type of person here and we are supposed to address all diversities. I want you to make more efforts.

E. M. Mong'are: Asante sana. Yangu itakuwa juu ya Rais. Majina yangu naitwa Elkana Monyoncho Mong'are. Kwanza kabisa, mimi ningetaka mtu ye yote anayeng'ang'ania uraisi awe kwanza ame declare his wealth.

Pili, awe ni billionaire ili tuweze kupoteza corruption.

Com. Adagala: Nikuulize, na kama alikuwa billionaire by corruption?

E. M. Mong'are: Ni awe ame declare vile alivyopata mali yake kwanza.

Com. Adagala: Kwa sababu anaweza kuwa billionaire by corruption?

E. M. Mong'are: That is very true.

Com. Adagala: Yes, endelea.

E. M. Mong'are: Pili, Rais lazima awe chini ya Sheria na sio vile ilivyo wakati huu.

Tatu, education standard yaani upande wa kimasomo. Pia, Rais awe ni mtu ambaye amefikia kidato cha nne na kwenda mbele, sio mtu ambaye atakuwa ni chini ya hiyo kiwango kulingana na maoni yangu.

Nne, Waziri ye yote atakayepolekwa mahakamani akiwa ako na case ye yote mbele ya mahakama ni awe suspended hadi wakati koti itakapoamua case yake na mali yote kama magari na vitu vingine

Com. Salim: Zamahani Bwana Mong'are. Ni Waziri peke yake?

E. M. Mong'are: Huu ni upande wa Waziri pamoja na Rais. Ikiwa ako na case mahakamani.

Com. Salim: Peke yao?

E. M. Mong'are: Kwanza ni pekee yao. Rais na Waziri. Hadi wakati mahakama itakapoamua case zao, ndio waweze kuendelea na nyatiba zao.

Tano, uteguzi wowote unaofanywa na Rais kwa watu kwenda katika ofisi kuu za serikali kama vile ilivyo wakati huu, uondolewe na hiyo juhudi ipewe Bunge ili iweze kuwa inateua wale watakao shikilia nyatiba hizo katika maafisi hayo.

Sita, nchi hii inafaa iwe na Prime Minister, ambaye atakayeteguliwa na wajumbe walioteuliwa.

Saba, nchi hii inatakiwa kuwa na coalition government. Hii iwe inauzisha viama vyote vya kisiasa vilivyoandikishwa. Hii ni kumaanisha kwamba, ikiwa Waziri ametoka katika DP, Waziri ametoka katika Ford People, Waziri ametoka katika KANU, iwe ni namna hiyo ili waweze ku share the cake equally.

Com. Adagala: Viama vyote arubaini na nane?

E. M. Mong'are: Vyote arubaini na nane ikiwa vinawakilishi katika Bunge.

Com. Adagala: Okay

E. M. Mong'are: Tisa, nchi hii inafaa iwe na a supreme court ambaye mwananchi wa kawaida anaweza kwenda mahakama na kuishtaki serikali iliyo uongozini na hiyo koti ipewe uwezo wa kuweza kui dismiss. Kwa kuweza ku dismiss hiyo serikali ikiwa itapatikana iko na makosa.

Nikitaka kuzungumzia upande wa insecurity in this country. Hii, ninaonelea vyema serikali irudishe maafisa wote wa Polisi, wa Jeshi, waliofutwa kwa makosa madogo madogo kwa sababu hao watu hasa ndio wanaousika katika visa vya ualifu. Warudishwe na wapewe contracts katika hizo departments sababu baada ya kukosa kitu cha kukula, huwa wanakuwa tempted kwenda kujiuzisha katika visa vya wizi.

Com. Adagala: Sasa wapewe reward?

E. M. Mong'are: Wapewe contracts za kufanya katika department ...

Com. Adagala: Ndio tunasema mtu ambaye amefanya uhalifu, sasa apongezwe na apewe kazi?

E. M. Mong'are: La! si hivo. Wale ambao hawajauzika katika visanga kama hivyo. Warudishwe. Wale ambao walitolewa kabla ya miaka yao kufika.

Na, pia ningependa muda wa Rais uongezwe kutoka miaka mitano hadi sita ikiwa pia term zao kung'ang'ania urahisi iwe ni mara moja tu bali si mara mbili kama Sheria inavyosema wakati huu. Muda uongezwe kutoka tano hadi sita na iwe ni mara moja tu!

Com. Salim: Muda wa Rais?

E. M. Mong'are: Muda wa Rais, iwe ni mara moja tu wa miaka mitano hadi sita. Kwa hayo machache, ninamalizia hapo.

Com. Salim: Asante Bwana Mong'are. Sasa namuita Bwana Mbeka Daniel. Joseph Kiarie, nafikiri hayuko huyo. Stephen Juma. Stephen Juma yuko? William Owino.

Speaker: Mimi nilikuwa tu na jambo moja la kusema tu. Nilikuwa ninaonelea.

Com. Salim: Jina lako tafadhali!

Speaker: Jina langu ni Stephen Juma. Nilikuwa ninaonelea hii bill ya family protection ipitishwe Katiba Bunge na ikuwe law. Halafu, watoto pia wawe wanaweza kujitetea kwa koti. Na kuongezea hayo, serikali iwe inaweza kushugulikia watoto wapate masomo ya msingi iwe ni free kwa sababu ya vile hali ya uchumi iko katika hii Kenya yetu sasa. Ni hayo tu, asante.

Com. Salim: Asante. Mara ingine tena, William Owino, tunaita jina lake.

William Owino: Mimi naitwa William Owino na mimi ningependa zile mamlaka za Rais zirudishwe chini. Halafu, ya pili, ningependa Mayor achaguliwe na Wananchi si ma-Councillors vile iko sasa. Ya tatu, ningependa yaani hao ma Polisi wache kushikashika vijana ovyo ovyo mbele hakuna kazi. Wakipata wamekaa chini, wanawashika bila kosa yo yote, kwa hivo, hii mambo ya Polisi kushikashika vijana ovyo ovyo ndio...

Com. Adagala: Akina nani?

William Owino: Polisi. Ya nne, ningependa Kenya tuwe na Majimbo system. Yangu ni hayo tu machache.

Com. Salim: Asante sana Bwana William Owino kwa maoni yako. Philip Oduor.

Philip Oduor: Yes, majina yangu ni Philip Oduor na maoni kuhusu Katiba ya kwamba iwe Government ikimaanisha the word 'NO', ikuwe 'NO'. Wakimaanisha ya kwamba hakuna kufanya kitu mbaya, iwe ni hivyo, for instance, kama vile walikataa

mambo ya kufaa hizi manguo kama 'macombat', unapata Rais anasema kwa mfano wamekataa vijana wasifae 'macombat' na bado unafind out ya kuwa hizi vitu zinaendelea kufanywa. Sasa, unashindwa kama Rais mwenyewe ndiye anasema, na haitili maanani, kwani Sheria yake iko wapi sasa?

Ya pili, unakuta kama mambo hii yenye ilisemekana ya kwamba ma tinted windows zitolewe mara moja na vitu zenye hazifanywi. Sasa tunataka sheria imaanishe chenye inatakikana iwe.

Ya tatu, tutaonelea ya kwamba kwa ma Constituencies zifanyiwe sub-division. Vile unavyoona ya kwamba a leader kama M.P. ni mtu anasimamia raia. Na vile anavyosimamia raia inatakikana ya kuwa awe ni kiwango cha raia wake kama ni 5,000 atakuwa amejua ya kwamba he is catering ama anasimamia 5,000 sio eti Constituency ingine inakuwa na raia 1,000, Constituency ingine inakuwa na raia 10,000 na wote wana serve kazi same. Yawe wanaangaliliwa kiasi cha watu wenye wanasimamia, unasimamia binadamu, sio land, ati sijui kilometres ngapi ndio unasimamia. Sasa zile kubwa kubwa zenye ziko na watu wengi, ziwe sub-divided.

Ya nne, ninaongea kuhusu Police harassment and brutality. Sasa hapo unajua tunaongea kuhusu hiyo harassment na brutality. Unakuta wanakuja kwa estate, wanashika watu.

Com. Salim: Sasa jambo hilo au tatizo kama hilo, tufanye nini?

William Oduor: Okay, kitu yenye ifanywe, waweke sector fulani ile yenye inasimamia raia ili wajue ma rights zao kwa sababu tunapata ya kwamba wengi wana suffer kwa sababu ya kukosa kujua rights zao. Bila kujua rights zako, unaweza kufanyiwa anything.

Ya mwisho, ni hiyo system ya Majimbo. Imenifurahisha sana kwa sababu nimejua ya kwamba kama kutakuwa na hiyo competition kabisa kwa kila Province, at least watu watapata kuendelea or development. Thank you.

Com. Adagala: Unatarajia ikiwa Majimbo, iwe Majimbo ngapi? Have you done arithmetic on that?

William Oduor: Iwe tu per the number of provinces.

Com. Adagala: Now existing?

William Oduor: Yes.

Com. Adagala: Okay, asante.

Com. Salim: Wycliffe Omondi.

Wycliffe Omondi: Kwa majina naitwa Wycliffe Omondi. Na naweza kupenda Katiba yetu ya Kenya ibadilishwe kwa vitu ambazo nitasema hapa.

Kitu kama music piracy. Nawezapenda serikali yetu ikuwe na/there should an enactment of a law in Parliament that safeguards the interest of musicians and artists. There should be no selling of pirated music compacts on the street, street vending and street hawking.

The Mayor of our cities like Nairobi, Kisumu and their deputies should be elected directly by the public and not fellow Councillors.

Police brutality. Before a Policeman arrests you, he should identify himself as a Police Officer by producing a card that will identify him to be a Police Officer instead of arresting you, taking you to Police cells, then

There should be a law that safeguards the right of a child in Kenya. In Kenya, we have got such cults like Mungiki which are causing public terror, in fact they are terrorists. There should be a law in Parliament, our MPs should enact a law that safeguards the interest of we Kenyans from such cults.

Then our rents. Our MPs should see to it that our rents are being regulated. There are some sizes of our houses or rooms or rather people like us who are staying in the 'gettos' which are very expensive. Our MPs should sit down na waone kiasi fulani ya room fulani isizidi kiasi fulani ya rent fulani. There should be a law that safeguards us tenants from not paying too much.

Com. Adagala: The Rent Tribunal is not doing that?

Wycliffe Omondi: The Rent Tribunal is doing a good job but

Com. Salim: Do you need another or do you need perhaps the same body in a different form like the Tribunal? What are the weaknesses of the Tribunal?

Wycliffe Omondi: Okay, they have not been doing their job well. We just need our MPs to put some pressure.

Com. Adagala: As you are living in town, you are living under Councillors, you also voted for Councillors, they should not be

it?

Wycliffe Omondi: They should.

Com. Adagala: I am asking you, should they be involved and how?

Wycliffe Omondi: Okay because Councillors are the most people – wale ambao wako karibu na Wananchi kushinda MPs. They should deal directly with this Rent Tribunal so that we tenants, tusilipe zaidi.

There should be free primary education.

Our President should be ceremonial and should be the Head of State.

We should have a Prime Minister who should be the Head of Government and should be elected for a period of five (5) years by fellow Members of Parliament. He should also be an M.P.

We should have a coalition government representing the interest of all Political Parties inside our Parliament.

Our Government should look into ways in which it will be creating jobs for the youth because we are the leaders of tomorrow so that we cannot enter into bad things.

There should be equal distribution of land to the landless, and the so called ‘machokaras’ or street boys, there should be rehabilitation centres – ile ambayo Government ndio ime set up of which watakuwa wana offer services like counselling and offering them education.

There should be proper drainage system (drainage system should be improved) so that the rain does not cause public havoc.

Thank you.

Com. Salim: Thank you Wycliffe. George Kamanda.

George Komanda: Mimi naitwa George Onyango Komanda. Nikitoa maoni yangu, naona ya kwamba kuwe na Sheria ambapo mtu ye yote ambaye anataka kuwania kiti ya ubunge ama diwani, lazima awe ni mkaaji wa eneo ambalo anataka kung’ang’ania. Isiwe mtu ambaye anatoka sehemu ingine, anaenda sehemu ingine kung’ang’ania ubunge ama udiwani huko na hajui shida za watu wa sehemu hiyo.

Jambo la pili, naona kwamba kuwe na kamati ya kuteua mawaziri. Isiwe ni jukumu la Rais peke yake kuteua mawaziri. Hii itafanya kwamba ama itasaidia kuwa mawaziri ambao wanateuliwa watakuwa ni watu professionals kama ni Waziri wa Elimu, awe ni mwalimu. Kama ni Waziri wa Afya, awe ni Daktari. Kwa hivyo naona kwamba kuwe na kamati maalum ambayo itategua mawaziri.

Jambo la tatu, naonelea kwamba uwezo ama mamlaka ya Rais ipunguzwe ili isiwe kwamba Rais ndiye Kamanda wa Majeshi, ndio Chancellor wa Universities zetu. Iwe kwamba kuwe na Chancellor wa University ambaye ni mwalimu ambaye ameitimu, kuwe na Kamanda wa jeshi ambaye pia lazima awe mwana jeshi ambaye amehitimu, isiwe ni jukumu ya Rais peke yake.

Jambo la nne, napendekeza kwamba kuwe na Waziri Mkuu ambaye atateuliwa na wabunge au kuteuliwa na chama ambacho kitakuwa kimepata wabunge wengi katika Bunge.

Maoni ya mwisho, naona kwamba, isiwe ni jukumu ya Rais kutangaza 'state of emergency'. Iwe ni jukumu ya Bunge, kama shida/vita katika sehemu mbali mbali nchini, iwe ni Bunge ndio ina jukumu ya kutangaza 'state of emergency'. Ni hayo tu, Asanteni.

Com. Salim: Asante George Komanda. Joseph Ochieng, Ameshandoka. Jared Otieno, Ameondoka. Wallace Nyariekko, Huyo amekuja kushikiza tu. Dismas Otieno Ojijo.

Dismas Otieno Ojijo: Kwa jina ni Dismas Otieno Ojijo. Mimi nataka kuchangia kuhusu hii Katiba. Mambo ya kwanza, ningependelea Chief achaguliwe na Raia sio serikali.

Ya pili, ningependelea mambo ya control ya kila kitu iangaliwe na serikali kwa maana tunaumia upande wa manyumba, chakula kwa maana juzi, iko wakati fulani President alisema kila mtu auze vitu yake vile anataka. Kwa hivyo sasa hiyo tunaumia sana. Unaweza kutu for example unaweza pata nyumba '10 by 10'. Mimi ni mkaaji wa hapa, naongea kile ambaye mimi najua. '10 by 10', unalipishwa 2,500/- na hiyo pesa hakuna. Kwa hivyo control kwa kila kitu iwe.

Jambo la tatu, corruption. Kwa maana sisi raia kawaida hatuna uwezo. Kenya imefikia pahali kama umekosa pesa, umevunja Sheria na ukiwa na pesa haujavunja Sheria. Kwa maana Polisi atakushika, na akuitishe kitu kidogo, akuache. Kwa hivyo sheria iangaliwe kabisa kuhusu mambo ya corruption.

Ya nne, tungependelea mambo ya elimu, watoto wasome bure kutoka nursery mpaka standard VIII. Iwe masomo ya bure.

Ya tano, mambo ya hospitali. Mtu anaweza kuwa mgonjwa, hana pesa kulingana na taabu ile ako nayo. Mambo ya hospitali, pendekezo yangu ni kwamba, hospitali iwe hata kama wewe mgonjwa, utibiwe. Utibiwe hata kama hauna pesa. I mean ni

bure.

Ya sita, ni kwamba serikali iangalie wale ambao wako na taabu kama watoto hawana Baba, maybe wako na Mama (street children), vile wanaweza kula na hata na kuvaa kwa maana hii ndio imechangia hii mambo ya uhalifu sana sana Nairobi hapa. Hawa watoto ndio wanapiga watu usiku. Pendekezo ni kwamba waangaliwe vile wanaweza kukaa, kupatiwa chakula na kuvalishwa na serikali.

Com. Adagala: Wazazi wa hawa watoto wako wapi?

Dismas Otieno Ojijo: Wazazi wa watoto? Unaweza kuta kama street children.

Com. Adagala: Nakuuliza, walizaliwa?

Dismas Otieno Ojijo: Yes, walizaliwa na wametupwa nje.

Com. Adagala: Na nani?

Dismas Otieno Ojijo: Na mama, maybe na mama.

Com. Adagala: Halafu, na baba ako wapi?

Dismas Otieno Ojijo: Baba unajua hao watu saa ingine wanapita kichoro choro. Baba amepotea, mtoto ako hapo.

Com. Adagala: Nataka kujua, kwa sababu unasema serikali. Na wazazi wafanywe je, hao wazazi wametupa?

Dismas Otieno Ojijo: Hao wazazi ambao wanatupa watoto wakamatwe, wawekwe ndani kama mtu amepatikana ametupa mtoto akamatwe awekwe ndani.

Com. Adagala: Itasaidia mtoto vipi?

Dismas Otieno Ojijo: Sasa akisha kamatwa, then, yule mtoto kwa sababu hajafanya makosa, yule mama au baba apate taabu huko ndani na mtoto asaidiwe na serikali. Sasa, wengine watapata adabu.

Com. Adagala: Okay, endelea basi, maliza.

Dismas Otieno Ojjo: Okay, namaliza. Namalizia kusema kwamba, napendekeza kuwe na Majimbo. Kulingana na Provincial level, kuwe na Majimbo. Asanteni sana, nimemaliza hapo.

Com. Adagala: Nataka kuuliza tu, chief awe elected.

Dismas Otieno Ojjo: Yes.

Com. Adagala: Na DO na DC.

Dismas Otieno Ojjo: Mimi napendekeza, DC awe anachaguliwa na serikali na DO na Chief achaguliwe na raia.

Com. Adagala: Okay, asante.

Com. Salim: Asante Dismas Otieno Ojjo. Vincent Asiro!

Com. Adagala: Kumeanza kuwa na kelele. Sijui hiyo desk isongeshwe.

Vincent Asiro: My names are Vincent Asiro. I am going to talk about the electoral (those who are holding public offices) especially very high offices like Chief Justice, the High Court Judges and Provincial Administrators. In the first place, offices such the Chief Justice's office and High Court Judges. We should have a panel to choose those who are holding such offices. They should not be appointed by the President but a panel that verifies and appoints. The panel should be set up by the Parliament.

If at all we have environmental laws in Kenya, they are not being implemented. We should have environmental laws that cater for the sustainability of the environment.

Com. Adagala: Excuse me! Excuse me. Mr. Wanjohi, please move that table or move those people from the door. Endelea.

Vincent Asiro: In Kenya, I think we should have some working environmental laws. Right now, our environment socially, physical environment is just in a mess. We should have working environmental laws in Kenya to deal with such things as pollution, planning of housing and utility of public places.

There should be special laws concerning the disabled, the youth, children and women in particular especially right now, they is nothing to do with laws working on the youth and the disabled and if at all they are there, I don't think they are being

implemented.

Secondly, something to do with corruption and fat guys. There should not be anything like being forgiven. There should be somehow a way to deal with those who committed certain crimes in the past that right now are afflicting Kenya. They should be prosecuted in some way.

Then, Provincial Administrators including our Mayors. They should be elected by the public. Secondly, you find that certain Political Party offices have been turned into administration offices especially KANU offices which I don't think should be the case. They are not our administrators, they are political leaders. Thank you.

Com. Salim: Thank you very much. We have listened to your views. We call now Michael Opinga.

Michael Obinga: Thank you very much Ladies and Gentlemen. I am Michael Obinga – Kasarani Youth Consortium. The following are the points that I have for today:-

I feel that in our Constitution, we should have a Preamble which should show clearly that the Constitution belong to the people of Kenya hence remaining under the people's custody.

Com. Salim: Mike, honestly there is no time for you to read. Just highlight the proposals or recommendations in it.

Michael Obinga: So, the people of Kenya should be the custodians of Kenya's Constitution. When we come to the Executive, he should be the Head of State, should not be a Member of Parliament. Qualifications of a President should be: He must be a Kenyan citizen, have attained the age of 33, a registered voter, must have served as a manager in a recognized firm for at least five years, his/her powers must be accrued from being a ruler to become a people's representative. He should make appointment of Cabinet Ministers which should be ratified by the Parliament. The Vice-President is just to be taking over from the President when he is away.

The post of the Provincial Administration should be scrapped to empower the Local Government.

Com. Adagala: What did you say about Vice-President?

Michael Obinga: The Vice-President should just have the qualifications that a President should have. He should not be a Member of Parliament but should be able to take over from the President when he is away.

Com. Adagala: Therefore he should go through the same process as the President – be elected

Michael Obinga: Yes.

Com. Adagala: By the

Michael Obinga: By the people.

Com. Adagala: Should he be a running mate of the President?

George Obinga: Yaah. Like for instance, he is a person from the Opposition. The second Party should take the post of a Vice-President.

Com. Adagala: So he is not a running mate? You see a running mate is the President and someone in his Party, okay and they both get elected on one ticket but a runner-up, what you are saying someone from the Opposition, a runner-up.

George Obinga: Yaah. A runner-up.

Com. Adagala: Is someone who has won the second highest. So, which one do you want?

George Obinga: I want a situation whereby somebody from the Opposition who is number two to be the Vice-President. The Provincial Administration, I feel should be completely scrapped off to empower the Local Government.

Cabinet Ministers: He/she should not be a Member of Parliament. Somebody to be a minister should not be an MP. Their appointment must be ratified by the Parliament. Merit-ocracy should be used. The President appoints the Cabinet Ministers but ratified by the Parliament. Kitambo kidogo tulikuwa na Minister for Education, Science and Technology. Siku hizi wamegawanyishwa mpaka hatuelewi mpaka tunakuwa na Ministers wengine hata hatujui wanafanya nini. There should only be one Minister, one Assistant, one Permanent Secretary and Assistant Permanent Secretary in one Ministry and we will also want to see a situation whereby a Minister for Education stands for Science and Technology not a situation whereby we have the Minister for Education, we have the Minister for Science and Technology, it doesn't make sense.

When we go to the Civil Service, the members of the Civil Service should be non-partisan. Their appointment to be ratified by the Parliament, their appointments by the President.

The Police should be non-partisan. Should ensure good security of the people. Professional ethics must be part and parcel of the officers in charge. Appointment of the Police Commissioner by the President ratified by Parliament, legislators should

Speak the voice of the people at all times. Their jobs as law-makers ...

Com. Salim: I have to take you back to Civil Service. You said the appointment should be ratified by?

George Obinga: By the Parliament.

Com. Salim: Each and every Civil Servant including clerks and messengers?

George Obinga: Senior people. So the legislators' job as the law-makers must at all times consult with their Constituents on relevant issues like for instance, when there is a bill in Parliament, people of Kasarani may want to see their representative coming back to them and asking them what to do according to that motion not just going and supporting what the Party is supporting. Maybe that is not what the Constituents want.

Com. Salim: Thank you Michael Obinga for your views. Ishmael Ishmael! Or he was only listening. Edwin Okello, Hayuko? Chrispine Odhiambo?

Chrispine Odhiambo: Asante. Kwa jina mimi naitwa Chrispine Odhiambo. Ya kwanza nitachangia juu ya elimu nikisema elimu iwe bure kwa Standard I-VIII na Philosophia yetu iwe "adui ya ujinga".

Ya pili nitaongea juu ya njaa kwa nchi yetu ya Kenya. Serikali itenge mashamba inayowesheza kulisha wa Kenya wote wasihumie na njaa kabla hawajaangalia mambo ya cash crops na mtu akipatikana amekufa na njaa, Rais aachishwe kazi na iwe kwa Sheria.

Ya tatu. Nitachangia juu ya uchumi. Sheria iwekwe ya kulinda waajiri na wanaoajiriwa. Kila M'Kenya ajue haki yake ya kazi ili anaweza kuchukua hatua kisheria kwa tajiri akitaka kumnyanyasa. Pesa ya chini kabisa kwa Wa'Kenya wanaoajiliwa iwe shilingi elfu nane.

Kwa Idara ya Polisi. Tunaomba iwekwe Sheria na iundwe kikozi maalumu wanao deal na Polisi na kila Polisi awe tayari kujitambulisha akienda kushika mtu. Kuanzia juu kwa kofia mpaka chini, iwe na namba inayoonekana wazi.

Upande ya judgement. Tunaomba Sheria iwekwe kwa serikali. Serikali alipe walalamishi wakishinda kesi yao dhidi ya wizi au uharibifu wa bidhaa zao juu washtakiwa hupigwa fine, au hufungwa jela na hufanyia serikali kazi.

Com. Salim: Twende nyuma kidogo. Ulisema tuweko na kikosi ambacho kitaangalia Polisi. Kikosi gani na kitachaguliwa na nani?

Chispine Odhiambo: Hicho kikosi kiundwe kupitia vile kikosi cha Polisi kiliundwa, ndio hicho kikosi pia kiundwe na station iwe tofauti.

Com. Salim: Na kitakuwa chini ya nani?

Chispine Odhiambo: Kikosi hicho ikiundwa, hata kikiwa chini ya Commissioner lakini bora station yao iwe tofauti mbali na Polisi kawaida.

Com. Salim: On the same point, kikosi hicho, hasa kazi yake itakuwa ni nini, kukuweka wazi?

Chispine Odhiambo: Kikosi hicho kazi yake, raia anaweza kupata mahali ya kushtaki Polisi akimtendea ama akimfanyia makosa.

Com. Salim: Unajua ukisema kikosi, mtu anafikiria another force, sio? Another group of armed people?

Chispine Odhiambo: No.

Com. Salim: Lakini ikiwa labda ni kamati

Chispine Odhiambo: Hapana. Kama kwa Jeshi tunapata kuna Military Police.

Com. Salim: Okay, na kikosi hiki kitakuwa ni chenye silaha?

Chispine Odhiambo: Kikosi hicho, watafunzwa vile wanaweza ku..... juu ukitaka kushika mtu, lazima ujue ujuzi wako wa kushika huyo mtu. Sasa Polisi ana ujuzi, nao pia lazima wawe na uchuzi ya kuchunguza mienendo ya maaskari.

Com. Salim: Maana kikosi cha kufanya uchunguzi?

Chispine Odhiambo: Ndio.

Com. Salim: Kazi ya Polisi?

Chispine Odhiambo: Ndio.

Com. Salim: Haya, endelea.

Chispine Odhiambo: Upande wa uongozi, naomba Sheria iwekwe kwa Rais awe ni mtu ana bibi mmoja tu lakini tunaomba yule atang'ang'ania uraisi awe ni mtu ana bibi mmoja. Na achunguzwe kama ni tajiri, ijulikane vile alivyotajirika, asiwe mtu aliye...

Com. Adagala: Twende hapo kwa Rais.

Chispine Odhiambo: Yaah.

Com. Adagala: Akiwa ni Muislamu awe na mke mmoja?

Chispine Odhiambo: Ndio.

Com. Adagala: Na dini yake inamuruhusu wane.

Chispine Odhiambo: Lakini hii ni Sheria ya Kenya sasa.

Com. Adagala: Pili, nataka kuambia watu wa Mathare hii si Political Rally eeh, hii ni Tume. Akiwa Mwanamke awe na mme mmoja pia, Rais akiwa Mwanamke?

Chispine Odhiambo: Na Mwanamke imejulikana anakuwa na bwana mmoja.

Com. Adagala: Haya.

Chispine Odhiambo: Achunguzwe vile alivyopata mali zake. Akipatikana kama na njia ya ufisadi ama kama alipora mali mahali ye yote.

Habari kwa manyumba, tunaomba hizi manyumba tunayoishi ziwe under City Council na wale waliofaidika wakajenga plot zao, Sheria iwekwe kali wawache kunyanyasa tenants. Ni hayo tu.

Com. Adagala: Ya nyumba.

Chispine Odhiambo: Eeh.

Com. Adagala: Sema zaidi kidogo.

Chripine Odhiambo: Nimesema nyumba za miji ziwe chini ya City Council. Yaani City Council wawe wakijengea watu nyumba ya kuishi.

Com. Adagala: Nyumba zote za

Chripine Odhiambo: Za mji.

Com. Adagala: Okay.

Chripine Odhiambo: Na wale waliofaidika wakajenga plot zao, Sheria iwekwe kali waache kunyanyaza tenants. Ile akiamka asubuhi, kesho nimeongeza mia tano juu ya ile unajua. Usipoongeza, hama.

Com. Adagala: Okay. Mtu akijenga nyumba, mwenyewe aishi na nyumba zote ambazo ziko rented ziwe chini ya City Council?

Chripine Odhiambo: Ndio.

Com Adagala: Vile tulivo sasa, itakuwa aje kwa wale wamejenga na wako Landlords? Ikiwa tubadilishe, tutafanya nini?

Chripine Odhiambo: Ndio nasema, nikisema waliofaidika wakajenga plot zao na watu wanakodesha, Sheria iwekwe kali wa wache kunyanyasa wapangaji.

Com. Adagala: Okay.

Com. Salim: Isaac Zadio.

Isaac Zadio: Asante sana. Kwa jina mimi naitwa Isaac Zadio, natoka hapa Mathare. Jambo la kwanza nataka niongee ni kuhusu kazi. Unapata mtu mmoja ni director pahali fulani, pahali fulani yeye ni chairman, pahali fulani yeye ni board member. Inafaa mtu mmoja awe tu na kazi moja sio ati mtu mmoja ana kazi tatu-nne-tano hivi.

Jambo la pili kuhusu kazi, unapata sisi vijana tumeenda shule, tumemaliza shule, tumeenda college lakini ikifika wakati wa kutafuta kazi, unaambiwa tunataka experience ya five years. Mimi naye ndio nimemaliza shule, ndio nimemaliza college, sijawai fanya kazi ye yote. Na nikienda kutafuta kazi, ninaambiwa unakiwa job experience ya five years. Hiyo haifai iwe hapo.

Com. Salim: Point zako, nakuambia, pendekezo lako ni nini? Tufanye nini?

Isaac Zadio: Nataka iwe ati, nikimaliza shule, nikimaliza college, nipate kazi. Sio ati ninaambiwa ati ninatakiwa na experience.

Com. Salim: Endelea, endelea. Saa yako inaendelea.

Isaac Zadio: Rais anafaa aende kwa term moja tu. Five years na iwe moja tu sio ati anaenda mara mbili. Halafu, Vice wake, inafaa iwe the runner-up. Number two kwa elections ndio anafaa awe Vice.

Halafu Mayor pia, anafaa achaguliwe na Wananchi sio ati na ma Councillors.

Halafu nataka Sheria iwe, wenye wako na mali sana, tuseme mtu ako na million tano kwa account yake, inafaa percentage ingine, tuseme 5% inakuja kwa watu ambao ni maskini. Halafu kuna watu wengine, ukiangalia tuseme hapa Mathare North, kuna spaces zingine zilikuwa zimebaki wazi, na sasa, zime grabbiwa. Nataka Sheria iwe, kama ume grab ardhi, hiyo ardhi ichukuliwe hata kama ushajenga, ichukuliwe na iwe kwa serikali.

Halafu, Polisi, sisi vijana Polisi wanatunyanyasa sana. Tukiwa kwa bara bara, unapata Polisi amekuja, amewashika. Anaenda huko kuwashtaki ati ulikuwa na bhangi, ati wewe ni suspect, wewe ni suspect wa bunduki, na hujafanya chochote, wewe ulikuwa tu. Mulikuwa munapumzika tu kwa bara bara. Hiyo haifai iwe. Halafu, tukiwa tu hapo bado, mtu akishikwa, unapata mtu mwingine anapelekwa remand anamaliza huko four years. Remand mtu haifai amalize, kama ni mingi, mimi nataka mtu amalize only one week kwa remand halafu kesi ianze sio ati anamaliza huko wiki mbili, wiki tatu, mwaka, mwaka mbili, four years, hiyo haifai iwe hapo.

Halafu mambo ya rent pia. Inafaa hii Tribunal haifanyi kazi. Rent Tribunal hawafanyi kazi, wanalala tu. Tunanyanyaswa hapa na ma landlords. Leo unalipa 1,500, kesho unalipa 1,800, next month atasema nimeongeza nyumba 2,000, na hajafanya chochote kwa nyumba. Hajafanya renovation, hajafanya nini na anaongeza nyumba, hiyo haifai iwe hapo.

Halafu ma MP wetu na Rais.

Com. Adagala: Unajua, hasa mambo ya mjini, mambo ya urban, ni nyinyi watu wanakaa mijini ndio watasema. Na mnasema, mnapitia pitia juu juu. Ni kama sio maisha yenu.

Isaac Zadia: Ni maisha yetu.

Com. Adagala: Hii mambo, kama ya Rent Tribunal, vitu kama hivo mnafaa msemee kamilifu kwa sababu mtu ambaye anaishi mashambani, hajui hayo mambo na kwa Katiba, nyinyi ndio mutasema. Sasa, Rent Tribunal kama haifai, nini inafaa?

Isaac Zadia: Wanafaa, lakini, inafaa wafanye kazi. Kwa sababu nakumbuka kuna nyakati tulienda kwa Rent Tribunal, watupee vile nyumba zinafaa zilipwe. Walituambia hawana chochote kama hicho wala hawajui. Walituambia chenye wanashugulika nayo, kama tenant na landlord wako na mvulugano, hapo wanaweza saidia lakini, nyumba ikiwa ni ya landlord, hapo analipishwa vile anataka. Haifai hivo, inafaa wachunguze rent inafaa ilipwe namna gani.

Com. Adagala: Generally?

Isaac Zadia: Eeh. Halafu tukikuja kwa hawa ma MPs na Rais wetu, yule ambaye anataka kugombea kiti wa MP, Councillor, u Rais, wao waende kwa HIV Test kwanza. Tujue wenye wanatuwakilisha huko sio wagonjwa ati wako na HIV.

Halafu, kuna kitu ingine hapa pia. Bill ikiwa kwa Parliament, inafaa MP wetu akuje, atuulize, hii bill, hiko hivi na hivi, tuifanye aje? Niende ni-i-support au niende nisii support? Au unapata bill pale, hao ndio wanajifanyia tu, bila sisi kujua. Asante sana, niko tu na hayo machache.

Com. Adagala: Sasa hawa wakifanyiwa tests, na baadaye waje kuonekana wako na HIV, itakuwaje?

Isaac Zadia: Anatolewa immediately.

Com. Adagala: Hii HIV Test, unataka iwe mara ya kwanza tu, wakati wanataka kugombea?

Isaac Zadia: Inafaa iwe yearly. Akikaa anataka kugombea, anaenda test, the first year ikiisha, anaenda test, second year, hivo hivo, mpaka muda wake iishe.

Com. Adagala: Okay.

Com. Salim: George Onyango. George Onyango? Ametoka. Fredrick Odhiambo.

Fredrick Odhiambo: Asante sana Commissioners. My names are Fredrick Odhiambo Kapele. The following are my proposals towards the Constitutional Review Commission:-

First, education should be the old system – 7-4-2. Basic education should be free. Government to control fees for ...

Com. Adagala: Why the old system?

Fredrick Odhiambo: I think the new system has been giving the children a lot of time and as compared to the old system, it is not producing mature outcome as the old system.

The Government should control fees for secondary and higher education in case they introduce the higher education i.e. there should be a minimum fees control in schools. University students...

Com. Adagala: That is there now.

Fredrick Odhiambo: That is still under the...

Com. Adagala: The control is there as a minimum.

Fredrick Odhiambo: There should be a fee in secondary schools and higher education

Com. Adagala: Yes there is. Why would you like beyond that?

Fredrick Odhiambo: Although it is, they should reduce. Although it is, by now but it is too high for some parents to afford. So, they should put a minimum stage so that the poor people can afford.

Com. Adagala: Okay.

Fredrick Odhiambo: Then, the University students should be given loan equally. This time although they are getting loans but most of the students are not getting enough to afford pursue their studies.

Com. Adagala: Excuse me, loans for whom?

Fredrick Odhiambo: The loans are not given in an average manner. Some are getting more, others are getting less. So, it should be given equally to the students who have applied.

In the issue of the National Hospital Insurance Fund (NHIF), there should be a law that when someone retires or is sacked before or when he never got sick and admitted in the hospital, the man should or the hospital should consider his contribution and should he be given chance to use the money if he is not working or if he dies, the beneficiaries should be given back the

money just like National Social Security Fund (NSSF).

A law should be given so that the Rent Tribunal cooperates with the National Housing to control the price of the houses just as the people had said. The houses are small and the rents are too high. So there should be a minimum charge to be paid for example, the smallest rooms like '8 by 8' be charged 800/- instead of 2,000/-. The conditions of the houses should also be looked at because some people are building houses without the toilets, some are building storeys without using the pillars which is so dangerous, some are built near the rivers. So, these should be looked at before the houses are rented.

Com. Adagala: You are satisfied with the size of houses?

Fredrick Odhiambo: Yes I am satisfied. '8 by 8' with 100 is okay.

Com. Adagala: I don't want you to link it to rent. I am talking about size of the house.

Fredrick Odhiambo: Yes.

Com. Adagala: You are satisfied with '8 by 8'?

Fredrick Odhiambo: Yaani, that should be the smallest. So, it can '10 by 10' or '15 by 15'. Also, there should be a law empowering the Kenya Bureau of Standards to check the standard of goods before they are sold to the common people because most of the business people are selling sub-standard goods to the common man. For example, here in Nairobi Estates, most of the chemists are selling generic medicines instead of the original. So, also this should be looked at.

Com. Adagala: You know that generic is cheaper?

Fredrick Odhiambo: Yes, but...

Com. Adagala: No, I am just saying you know that?

Fredrick Odhiambo: Yes, they are cheaper. There should be a law to control the prices of goods.

Com. Salim: Fredrick! You know that banging means that your time is up. Can you please wind up now.

Fredrick Odhiambo: There should be free medical services at the basic level, that is, dispensary level while as from the district level, the charges should be reduced.

The power of the President should remain the same but his duties to be reduced. Thank you.

Com Salim: Thank you Frederick Odhiambo. Now, I call Joseph Kihara. Joseph Kihara! Hayuko. Joseph Kihara Gitunda. Beatrice Atieno! Huyo ni bibi wa kwanza kabisa leo kutoa maoni yake. Na kama wenzangu aliposema hapo hawali, ningependa wako waweko kina mama wengi kutoa maoni yao ingawa sioni wengi, ni kiasi cha wale watano tu. Let us hope kwamba baadaye tutapata kina mama wengine. Beatrice Atieno, tafadhali utaanza kwa jina lako.

Beatrice Atieno: Kwa jina naitwa Beatrice Atieno. Katiba, sijui kama ni kugeuza ama ni kuongezea, sasa ningependa ile Katiba ambayo ilikuwako, hizi matangazo ambayo mmeandika huku, pia ni pesa. Sasa ile Katiba ambayo tuko nayo, mngeandika hata at least ilikuwa hivi, hiko hivi. Sasa naweza kuja nisome pale niseme, hii, haitusaidii, nataka iwe hivi.

Na nikiongezea hapo, sasa tukisema tunataka watoto wasome bure. Hatujui kama ilikuwa kwa Katiba ya zamani ama sisi ndio tunataka kuiweka. Kama iko, iwekwe.

Com. Salim: Bi Beatrice, si lazima kitu kiweko kwenye Katiba hii tuliokuwa nayo sasa. Sema hata ikiwa jambo lipya, liko si liko, wewe ungependelea, utalisema.

Beatrice Atieno: Si mutaandika makaratasi nyingi sana. Ikiwa iko, tunarudia kwa sababu sijui ile ilikwako.

Com. Salim: Nasema aje Beatrice, hata ikiwa haiko, ndio unataka elimu iwe bure, sema.

Beatrice Atieno: Nataka elimu ya msingi iwe bure. Ningependa pia, ma hospitali ya City Council, itibu watu bure hata Kenyatta pia itibu watu bure. Na kama ningejua ile ilikuwako, ningesema mengi. Saa hii sina mengi. Asante.

Com. Salim: Beatrice amesema mambo muhimu sana. La kwanza alilosema ni kwamba hajui yaliyomo katita Katiba hii tuliyo nayo sasa. Sisi, tulianza hii kazi kitambo sana zaidi ya mwaka sasa. Na jambo la kwanza tulilotaka tufanye, ni kuelimisha Wananchi juu ya Katiba tuliyo nayo hivi sasa. Na imeonekana wasi kwamba hapa Kasarani, civic education imekuwa na matatizo, kuonyesha kwamba haikufanywa kwa njia ambayo inapasa kufanywa. Na hilo ni kosa, tunawataka radhi kuwa hatukufanya kazi hiyo kama ambavyo yapasa ifanywe. Lakini hata hivo kama nilivyosema, mtu aseme yale matatizo yaliyoko na juu yake aeleze, anataka tufanye nini. Katiba mpya, si lazima tupadilisha ile ilikuwa tu lakini tanaweza kuongeza vitu hata ikiwa havimo Katiba ya sasa, muktaka, munaweza kupendekeza yawemo katika hii mpya.

Na pili, mwenzangu ananikumbusha kwamba kuna haja ya utulivu ili tusikize vizuri yale yanayosemwa. Asante.

Sasa namuita Bwana Shem, Omwani Diki.

Shem O'Mwandiki: Asante sana. Mimi ni Shem O'mwadiki na nitaongea kwa hapa Nairobi na Kenya mzima. Asante.

Ya kwanza, Kenyatta National Hospital zamani ilikuwa bure. Na sasa ni pesa, sababu gani, inaumiza raia.

Ya pili, inaonekana katika serikali yetu.....

Com. Salim: Ungependelea nini habari ya Kenyatta Hospital au hospitali nyingine? Sisi tunaandika Katiba kwa watu wote wa Kenya, wengine wako Mombasa, Kisumu na kwingine. Tusifikirie Kenyatta Hospital peke yake.

Shem O'Mwandiki: Okay. Ukisikia nikisema Kenyatta Hospital tena iko Mombasa, iko Nakuru, kila mahali, kwa hivyo iwe free. Na ikiwa wanataka private ijengwe tu kando na tujue ni private, hiyo ni ya pesa. Mbona ilikuwa ya bure sasa ni pesa, raia wanakufa ovyo ovyo hata ndani ya hospitali hiyo.

Com. Adagala: Unajua Shem, sasa sio wakati wa maswali. Sasa ni wakati wa mapendekezo. Pendekeza.

Shem O'Mwandiki: Pendekezo langu iwe free? Sawa?

Com. Salim: Uendele.

Shem O'Mwandiki: Ya pili, tuna serikali yetu ya Kenya inaendelea na kazi sawa sawa lakini wanalia sana ati kuna wizi na kuna Polisi. Kazi ya Polisi ni nini? Kama Polisi ni kidogo, waongeze watu wengi kwa sababu hawana kazi.

Com. Adagala: Unajua inaweza kuwa ni style yako ya kuzungmza lakini tunataka pendekezo. Sio maswali.

Shem O'Mwandiki: Pendekezo langu waongeze askari wawe wengi, kazi iendele.

Ya tatu, umaskini na bado wanaumia. Pendekezo langu liko kuna ma tajiri na masikini, na tunataka watu wawe sawa sawa. Kila Mwafrika ambaye aliye katika Kenya, hata ikiwa ni million therathini, kila mtu awe akipewa million moja kufanyia business yake, tumalize umaskini.

Nikiendelea, harambee inapofanywa, inasaidia ma tajiri, haisaidii maskini lakini wakitoa hiyo million moja kwa kila mtu, Kenya itakuwa sawa kabisa.

Nikiendelea, inafaa waze wa vijiji wapate mshaara sababu wanafanya kazi kubwa sana mbele ya serikali. Vile councilor wanapata, wazee wa vijiji wapate kama wafanya kazi wengine wa serikali.

Niendeleo, kazi ya masomo. Shule zinakuwa chache katika estates na tunahitaji watuongeze shule ziwe nyingi. Kama hapo Mathare North, hatuna secondary, ni moja tu pekee yake na hata kiwanja ya kuchezea mpira hakuna. Na katika estate ingine, kuna viwanja. Mbona hapa hakuna kiwanja hata kimoja. Hii inaonyesha ni matharau katika serikali yetu!

Shem! Nitakuambia mara ya mwisho. Hii si wakati wa maswali. Toa pendekezo safi. Nakuambia mara ya mwisho.

Shem O'Mwandiki: Pendekezo, shule ziongezwe. Ufisadi ni nyingi na serikali hiko, si imalize! Imalize kwa sababu hiyo ndio kazi yake. Halafu watulinde, na tufurahi na tuwe na nguvu, tukiamka tuwe na furaha.

Com. Adagala: Maswali yako imemaliza muda wako.

Shem O'Mwandiki: Kwa sababu ni mazuri. Asante.

Com. Salim: Asante Shem. Simon Ngatia nafikiri. Simon Ngatia, Mushroom Community, iko? Mary Goret. Zedekiah Orioki, Zedekiah!

Zekediah Orioki: My names are Zedekiah Migiro Orioki. I have five pertinent proposals.

I will start with Preamble. We need to have a Preamble in our Constitution and I propose, to open "We the people of Kenya".

Then, I propose our Constitution should have a vision which is geared towards poverty alleviation because we have the natural resources which are quite abundant but are not maximumly exploited and even utilized.

Then, in the Constitution of Kenya under the Preamble, I propose that the Kenyans who fought for independence should also be remembered as a matter of remembrance for generations to come.

Second proposal on Political Parties. I propose that Kenya needs to have at most three strong Political Parties. The reason being, many Political Parties are just like family undertakings hence they don't have the national look-out and also they cannot work as watch-dogs against a Political Party in power. Also, I propose that these Political Parties should be financed by the State and that their expenditures to be controlled whereby they submit their financial reports to the Auditor-General for the sake of accountability and transparency.

Then, I talk about electoral system. I propose that Presidential elections be divorced from Parliamentary and Civic Education

so as to minimize or avoid manipulation and also

Com. Adagala: The explanations are going to eat your time. If you say separate elections is fine. Go for your proposals directly so that you can make as many as possible.

Zedekiah Orioki: And also I propose that the counting of votes be conducted at the polling stations and not in one given counting hall. And also I propose that the ballot boxes be transparent.

International relations. It shouldn't be the work of the Executive alone. I propose that students who go outside this Country for further studies to undertake a mandatory one-year course on international relations so as to act as ambassadors wherever they are because they will have understood it better.

On the side of governance, I propose that it should be all inclusive together with our resources and NGOs and other organized groups to be also involved even when we are preparing the budget.

Lastly, I therefore propose that our Budget should be as per our income without expecting anything from without.

Com. Adagala: Okay, thank you. I wanted to ask you about the three Political Parties. Very many people are proposing this but we have freedom of association and freedom of speech. What shall we do with that because this is an expression of people themselves wanting to vote that way and we fought for Multi-Party.

Zedekiah Orioki: Alright. It is true that many Kenyans are really talking about freedom of speech, association but think of it, what is up? We fought for Multi-Party but since 1992 to-date, you find Orioki today together with a friend and a nephew going and registering a party and then you call a Political Party. You wonder, what is the essence of Multi-Party? It is to act as watch-dogs. So, what I am proposing Madam is like, in as much as that could be an infringement of the fundamental rights that we are talking about even in our Constitution, still, we must also be sure of the distance that we are supposed to cover as Kenyans, because if we had strong Political Parties even the small Parties can unite and then agree because it will be a law under the Constitution to come out with that.

Com. Adagala: How shall we arrive at three?

Zedekiah Orioki: I will suggest all those Political Parties already registered to be grouped because it will be a consensus. Like each Political Party has got, say, a Chairman or officials of that Party, they should come together and work out on the modalities such that we have at least a maximum of three major Political Parties in this Country.

Com. Salim: Thank you Bwana Orioki for your views. Nelson Ochieng, Nelson Ochieng!

Nelson Ochieng: Kuhusu Katiba yetu ya sasa, mwananchi (raia wa kawaida) hana nguvu kutoa maoni na maoni yake isikizwe na serikali. Kama tuseme tukishachagua Mbunge wetu, akienda huko tuone hatekelezi yale mambo ambayo anatakikana kutekeleza, sisi Wananchi wa kawaida huwa hatuna nguvu ya kumuita ama kumuona kumuuliza kwa nini ulitambia wakati ulikuwa unataka kura? Mimi ningependa mwananchi wa kawaida awe na nguvu hata baada ya kuchagua, ku pass vote of no confidence kwa yule Mbunge ambaye hatekelezi kazi yake.

Ya pili tena katika serikali yetu. Sisi Wananchi wa kawaida, hatuna nguvu. Maoni yetu, hata tukisema tunanyanyaswa na Polisi, maoni yetu haichukuliwi kama muhimu. Mimi napendekeza kwamba Katiba ambayo tutakuwa nayo sasa, ipatie mwananchi nguvu ambapo iwe na ile tume ambayo inachukua maoni ya Wananchi kuhusu utekelezaji wa serikali ama sector ingine ya serikali kama tukiona hii sector kama ya Polisi haifanyi kazi sawa sawa, wanachukua maoni ya Wananchi halafu wanaweza hata ku disband hiyo sector, waandikishe watu wake.

Basi, kwa sababu ya saa, asante.

Com. Salim: Asante sana Bwana Nelson Ochieng. Paul Oloba. Paul uko? Charles Nyario.

Charles Nyario: Asante. I have very crucial proposals to the Commission. My names are Charles Odoyo Nyario. The proposals that I have before you are:-

1. Denominations. I propose that we should have a few number of churches and denominations, that is, and before they are registered, they should be screened. This is going to control our abuse, that is

Com. Salim: I think you said about the churches have to be screened. By who? Who should screen them?

Charles Nyario: By the Registrar of Societies. This is going to control the blasphemy to God. They should be screened properly and because

Com. Salim: Did you say Registrar of Societies?

Charles Nyario: Yes.

Com. Salim: What has the Registrar of Societies to do with Judges?

Charles Nyario: Churches. Not Judges.

Com. Salim: Alright.

Charles Nyario: That is the denomination.

Com. Salim: Sorry sana.

Charles Nyario: Then, when I am coming to education. The education should be free and compulsory at primary level and it should be monitored (those who are not going to school), they should be monitored by local administrators.

When we are coming to security. I propose that the Police Officers found breaking law should be discharged from their duties without any benefits i.e. arresting without warrant, drinking while on duty, demanding bribes (that is TKK) from the offenders.

Then, when I am coming to people are employed in Forces like GSU, Kenya Airforce, Kenya Army. I propose that these people should be engaged in building our Nation, that is they should be engaged in infrastructures, building of roads, bridges, schools and government institutions. That is all.

Com. Salim: Thank you Bwana Charles Nyario for those views. David Otieno! Samson Oboke! Johnson Muthumbi! George Odhiambo! Pastor James O. Juma, E. M.T.C. Church.

James O. Mwajuma: My names are

Com. Salim: Mwenzangu amenikumbusha jambo. Hawa jamaa ambao tumewaita, wamejiandikisha kitambo na sasa hawako. Nafikiri tunaafikiana kuwa tuna watu wengi sana ambao wanaendelea kujiandikisha kutoa maoni, hatuwezi kurudi nyuma. Wakitokea, wasitulaumu kuwa walijiandikisha lakini hawajasikia majina yao maana mtu ametoka, amefanya kazi yake nafikiri kwa kurudi atashikilia ile pahala pake. Sisi tutaendelea mbele na hao ambao hawako na lao haliko, waswahili wasema “asiyekuweko na lake haliko”.

James O. Mwajuma: Jina langu naitwa James M. Wajuma. Pendekezo langu la kwanza, kwa upande wa equality. Upande wa equality, unapata kwa Biblia ya kwamba Mungu aliumba Adamu ya kwanza.

Com. Adagala: Tafadhali, toa pendekezo.

James M. Mwachuma: Thank you. Pendekezo langu ili mwanamke asitafute kutoshana na bwana, ile Sheria ipitishwe.

Pendekezo langu la pili, watoto lazima waadhibiwe, kwa sababu bila kuadhibiwa, watoto wanaweza kufanya vialifu. Watoto wafundishwe wakichapwa wakiambia ili ni kosa kwa kupigwa.

La tatu, Polisi waweze wakajua ya kwamba pasipo na Wananchi hawawezi kufanya. Kwa hivyo, lazima watipishe Sheria ya kwamba wasiulize mtu kitambulisho ambaye ni mtu wa Kenya ili waitishe hongo.

Upande wa kazi, napendelea ya kwamba, ye yote ambaye...

Com. Adagala: Wacha turudi hapo kidogo, watajua aje wewe ni mtu wa Kenya? Sasa, unajua Kenya watu huja wengi, wanatoka Rwanda, wanatoka Ethiopia, wanatoka Somalia, sasa watajua aje wewe ni M'Kenya?

James O. Mwajuma: Akishapata wewe ni mwana Kenya, akuaje utembe huru kwa maana unatembea kwa Nchi yako.

Com. Adagala: Vile atakuliza ni kitambulisho?

James M. Mwajuma: Atakuliza kitambulizo. Na akishathibitisha ya kwamba wewe ni mwana Kenya, akuache huru.

Com. Adagala: Okay.

James O. Mwajuma: Kwa upande wa kazi, unapata ya kwamba kuna ma directors, watu wengi kubwa kubwa. Akitaka kuandika watu wake, anafukuza watu.

Com. Adagala: Unajua, wacha niwaambie Mwananchi. Tunaweza kuwaweka nyote pale nje, na tuite jina moja moja kutoka kwa mlango, halafu mtu ataketi hapa peke yake bila hii kelele. Haya mambo, inawekwa twa tapes na tape hii itadumu, miaka hamisini, miaka mia moja. Hatujawahi kuwa na watu wengine kama nyinyi. Najua watu wa Mathare ni watu wa pekee lakini hii, ni kitu muhimu sana. Si rally, ngojeni Mheshimiwa ataita rally, mtaenda. Hapa mkimie, mbele ya Tume, ni mtu mmoja tu ako hapa, yule ambaye ameketi hapa. Tafadhali, na makofi makofi wekeni kando, utatoa maoni yako. Na ni mara ya mwisho kwa sababu ikiendelea, tutawaweka nje, tutaita mtu mmoja mmoja.

James O. Mwajuma: Upande wa kazi, napendelea ya kwamba mtu asiwe na Sheria ya ku retrench watu halafu anaandika watu wake. Hiyo mambo ya ku retrench watu halafu unaandika watu wako, ikome.

Upande wa Majimbo. Ninaonelea ya kwamba kabla moja limefaidika sana kwa ajili ya serikali ambaye imeungana pamoja. Na ikiendelea hivo, maoneleo yangu ninaona ya kwamba, Majimbo iwekwe.

Namba mne ya shida nikienda kumalizia. Hii mambo za night clubs within the estate should be abolished. Mambo ya night clubs...

Com. Adagala: Tafadhali Wananchi, atuwezi kusikia huyu mtu kama mnazungumza. Mukitaka tuwe na vita na nyinyi, tanaweza toa hakuna shida, lakini tuta clear the hall. Tunataka kusikia huyu mtu hapa na kila mtu atakuwa na zamu yake.

James O. Mwajuma: Pendeleo yangu ninaonelea kwamba haisitaili bars na night clubs iweko ndani ya estate (mahali watu wanaishi). Hiyo Sheria zipitishwe na kila bar isipatikane kwa estate.

Nikimalizia kwa upande wa NSSF. Watu wengi wanakufa kabla hawajapokea pesa zao walikuwa wakipeleka pale. Kwa hivyo, maoneleo yangu, ninaonelea ya kwamba ye yote akishawacha kazi, haisitaili afike miaka hamsini au hamsini-tano. Akishawacha kazi yake na anataka pesa yake, apewe hiyo na Sheria ipitishwe. Hiyo tu.

Com. Salim: Asante sana. Sasa tuna mwita Bwana Joseph Murunga, yuko? Mathare Progressive Youth Association, yuko mwakilishi kwa Chama cha Vijana cha Mathare Progressive Youth Association? Ameondoka. Japheth Alandi?

Japheth Alandi: My names are Japheth Alandi and the following are my proposals.

I would suggest that the Judicial Officers be appointed by the Law Society of Kenya (LSK).

Com. Adagala: Unataka checks and balances ambazo hatuna sasa. Huwezi kusema appointment by LSK itakuwa tu appointment by President, mtu akichagua, mwingine anachagua, unependelea nani achague?

Japheth Alandi: Maybe, let it be an election by the LSK.

Com. Adagala: We have agreed, do you want anybody else to look at these appointments?

Japheth Alandi: Yes.

Com. Adagala: Who?

Japheth Alandi: Maybe the Chairperson of LSK.

Com. Adagala: We have agreed appointment, there is something called vetting. Who would you like to vet?

Japheth Alandi: Let it be the CJ.

Com. Adagala: But he is also an appointee?

Japheth Alandi: Yes.

Com. Adagala: Okay. Let me leave like that.

Japheth Alandi: Again the councillors to have at least 'O' level qualifications and M.P.s remuneration should be controlled in relation to the economic situation of the Country.

Com. Adagala: By?

Japheth Alandi: By maybe a Task Force assigned by the Government. Then, the Electoral Commission should be an independent body appointed by the Legislators themselves but funded by the Government.

A law should be enacted also to protect the interests of the youth. Also....

Com. Adagala: I think you need to say a little bit more on the youth.

Japheth Alandi: Concerning their fundamental rights. The infringement of their fundamental rights. Again, the law should also be put in place to control the operation of the public service vehicles in terms of the charging of the fares. Then, also, a law should be enacted to control the code of behaviour of the Head of Public Institutions, State Parastatals and even the Corporations such that the law renders the heads illegal to run another state corporation after having misappropriated given parastatals funds.

And then the Corruption Control Board should consist of Non-Kenyan citizens but funded by the Government.

Com. Adagala: The what body?

Japheth Alandi: The Corruption Control Board should consist of Non-Kenyan citizens (headed by Non-Kenyan) but funded by the Government. Members will be Kenyans. A law should also be enacted towards restricting the transfer of wealth by Kenyans and foreign investors to their foreign states as an avenue towards poverty alleviation and economic recovery. Thank you.

Com. Adagala: What could be the advantage of having a Non-Kenyan to head the - you said corruption control?

Japheth Alandi: Yes.

Com. Adagala: Not anti-corruption?

Japheth Alandi: Yes.

Com. Adagala: You just want corruption control?

Japheth Alandi: Yes.

Com. Adagala: Not taken away/not eradicated?

Japheth Alandi: Whichever is the case.

Com. Adalaga: What do you want?

Japheth Alandi: I want corruption to be alleviated.

Com. Adagala: Okay, why should a Non-Kenyan head it?

Japheth Alandi: This will give him/her a chance to fully investigate the matter without fear. You know, if you are Kenyan and you may prosecute the front-stars and you stay in the country, you don't what will happen tomorrow. You are insecure.

Com. Salim: What about the Kenyan members?

Japheth Alandi: The Kenyan members, if you maybe expose somebody, maybe he is a very chief person in the Government, then after the exercise is over, you are insecure. You don't know whether you might be killed any time.

Com. Salim: Inaudible

Japheth Alandi: The members yes. But you know, that is why I have said they should just be members. If you are heading a team, it is the head that is looked at.

Com. Salim: Inaudible

Japheth Alandi: Yaah, but it is not as if you are the head.

Com. Salim: Now, James Odhiambo

James Odhiambo: Majina zangu kamili ni James Odhiambo. Kwanza kabisa, pendekezo langu la kwanza lingekuwa ya kwamba wakati Katiba inapopitishwa, lazima iwekwe katika sehemu ambayo mwananchi wa kawaida anaweza kuifikia na kuijua kwa sababu katika Kenya hii ya sasa, Wananchi wengi hawajui Katiba. Hata wakati tuko hapa tunapokuja kurekebisha Katiba, watu wengi hawajui hata Katiba ya kitambo ilikuwa ikisema nini.

Ya pili, mawizara. Katika Kenya hii yetu tunaona ya kwamba tuna Waziri wengi lakini Wizara ni chache na sijui ni kwa nini Wizara moja iwe inaongozwa na karibu Mawaziri watatu. Kwa hivyo ninaonelea kila Wizara iwe na Waziri mmoja na wale ambao wako wawili watatu, wapunguzwe.

Pendekezo la tatu ni kwamba, Rais anayekaa ama the sitting President. Inafaa wakati anapofanya makosa, apelekwe kotini. Hakuna Sheria yakusema kwamba ati Raisi hafai kupelekwa kotini. Na ninaona hivo pengine unyanyasaji wa raia wa kawaida utaisha.

Pendekezo lingine ni kwamba, Presidential appointees should be vetted. Yaani, ikiwa Rais atachagua Waziri ama Director kuongoza sehemu fulani, lazima kuwe na kikao fulani ambacho kitatambua kama huyu mtu anafaa katika hiyo kazi ambayo alipewa. Kama hawezi, basi, atolewe.

Halafu, pendekezo lingine is setting of Commissions that don't deliver. Kuna Commission ambazo zimesha setiwa mingi sana Kenya hii kufanya uchunguzi lakini ile matokeo ambao wamepata, sisi Wananchi wa kawaida, hatujawahi kupewa na ni pesa zetu zinatumika katika ku set hizo Commissions. Ikiwa hizi Commissions haziwezi kutoa jawabu, hazifai kuwepo tena.

The appointment of the CJ and the AG. Hiyo pia ninaona ya kwamba haifai kuwa Rais ndio achague hao watu kwa sababu anapowachagua basi, wale watu wakiwa pale watakuwa wakimtumikia tu yeye na sio Wananchi, kwa hivyo hao watu, wachaguliwa na members of the bench in conjunction with LSK na hivo itakuwa ni vizuri.

Halafu, upande wa Polisi sasa. Katika Kenya hii yetu tunaona kwamba, sisi Wananchi wa kawaida, Polisi hawatupatii ile treatment tunayoitaji. Tunapata kwamba ma tajiri wanapoenda kushikwa na Polisi, mara nyingi, Polisi

Com. Salim: Toa pendekezo, umetoa maelezo na kila ukitoa maelezo wakati wako unapotea.

James Odhiambo: Sasa nasema hivi, Polisi akija kunishika, ikiwa mimi ni lazima nitiwe pingu, basi hata yule tajiri anaposhikwa, pia yeye atiwe pingu hata kama ni Mbunge, hata kama in Rais. Ndio hiyo pendekezo langu. Pendekezo ni kwamba basi sisi zote tupewe usawa. Ikiwa mtu ni tajiri mwingine ni maskini, tupewe usawa sisi wote. Asante

Com. Salim: Asante sana James Odhiambo. Abdalla Onyango.

Abdalla Onyango: Thank you very much. My name is Abdalla Onyango and I have some views which I have to share with you.

First, I am going to talk about is Police brutality. The Government should form a sector which will deal with the Police brutality under Anti-Corruption Unit.

Second, Rent Tribunal. This body, we found that it is now existing but they are not doing their job. So, under new law, I would like them to wake up and do their duty or else we should disband this body.

Com. Salim: Which body is that?

Abdalla Onyango: Rent Tribunal.

Third, Mayoral post. This post

Com. Adagala: Who will be there? Because someone/something has to be there.

Abdalla Onyango: If it is disbanded, we will form a welfare for these tenants to deal with the rent.

Third, Mayoral post. This post, we the Wananchi are the right people to select this man who is going to represent us as the Mayor. So, it should be Wananchi to select.

Another one is education. Education in primary level should be free and compulsory and in university, according to me, if there is someone who cannot afford to get the funds, he should be given a loan and it should be a must that I have to be given a loan.

Laws in Kenya. Laws are there but not working. So, I would like these our laws to be strengthened so that they work.

Last, lawyers. These people, in short, maybe I got an accident and he is the one who is representing in court so as to be compensated. So, you will get the compensation will be made through the lawyer and I will end up not getting my portion. So, my side is the compensation should be done through me so that I can now give him his portion. Thank you very much.

Com. Salim: Thank you Abdalla Onyango. Next is P. L. O. Ongweny, yuko?

P. L. O. Ongwen: My right names are Ongwen Paul. So, the first recommendation is that civic education should be continuous so that the people can know their rights. You know, ignorance is no defence and therefore, if a new law is enacted, we should get to know it.

Com. Adagala: In what forms are you considering?

I

Paul Ogweny: Okay, it should continue as per the Constituency. So, these people who are carrying out this activity should continue with it. It should be continuous. Yes, through CBOs of course.

Then, I am talking about corruption where I am suggesting that they set up an office of the Ombudsman. A neutral person who is elected by the people.

Citizenship. I would suggest that we have a dual citizenship. If you are a man and you are a Mzungu and you have married a Kenyan, you should be entitled to the Kenyan citizenship. If you are a Mzungu lady and you are married by me (Kenyan man), you should also be entitled. Even a child whom we get, should be a citizen of Kenya.

About the youth, I was requesting the Government through the Ministry of Labour that a law should be enacted to protect the youth from the foreign employers who are always giving these people very little money. You know even if it is enacted that there is an increase, they don't always implement it. So, there should be a strong rule from the Ministry of Labour through the Workers' Organisation.

Com. Adagala: Who is a foreign employer?

Paul Ongwen: A foreign employer, I am talking of a Muindi from India who has just come here to invest. Are you satisfied? This Muindi is not a Kenyan. We know we have Kenyan Muindi but this is a Muindi from just India to come and invest in our Country and is now a foreign investor. He is a Muindi ambaye ananyanyasa watu wetu. That is the person I am talking about.

Com. Salim: Are you talking about foreign investors in general, whether it is a Muindi or Mzungu.

Paul Ongwen: Okay, let us put in general but employers wale wananyanyaza watu especially the foreign ones, hao ndio wabaya sana. I am stressing on this.

Now, I am talking about university students. Normally, the courses are not relevant to the labour market and therefore, I would request that the curriculum be overhauled. After overhauling it, the courses should be relevant. These students should get attachment with the relevant companies through the Government, through the Ministry of Education and the Labour Ministry.

Another thing for our youth, we should start something called an ‘employee benefit’ whereby these people who are getting big money, at least they can look for a way whereby their money can be taken at least kidogo kidogo so that these people who are not employed (they youth), at least they can be getting something kidogo to keep them going.

I would also mention something about soft loans especially to university students. They should be getting soft loans to start some micro-enterprises. This should also go to the other youth who are not university students. The Government should set up something like a micro-finance whereby organized women groups, youth groups and even men with their organizations, they can always draw some money, start small businesses and then, they will keep on training them how to man them.

I would mention something on prison conditions. You know, our prisons are meant to harden people. They are not meant to rehabilitate people. So, I would suggest that the conditions should be improved so that when you come out of prisons, you are now a clean man.

Again, there used to be a law called “burglars’ law”. This one where you are taken home if you are found loitering. I would suggest that, that law at least it should be enforced such that when you come out of prison, instead of coming back again to become a hardened criminal, you are taken back to your place so that even the people (Ja’luo na M’Kikuyu na M’Kamba) wale waliokuwa wanakaa pamoja na wanaiba watu, one is now in Ukambani, one is in Coast and the other one is in Nyanza.

I would talk of (just a minute Madam) this vulnerable group – the chokoras. I would suggest that the Government looks for a way of rehabilitating these boys. They should get proper education. They should get medicare and in fact they should follow it up with even their parents so that their parents can also be taken to task because most of them are prominent people like me and these people, some of them are working. So, these chokoras, they can be drawing some money from the parents (these people who are working) and then trying to rehabilitate these boys. I will just stop there for now, God bless.

Com. Salim: Thank you Bwana Ongwen. Eric Omondi, hayuko? Alice Sanya.

Alice Sanya: My names are Alice Sanya. First of all, I would like to make a proposal that, on the education strategy in Kenya. You find that the Government only takes care of those who have finished form IV, only those who qualify for university are invited to the universities but the Government is not taking care of those who missed the points to go to the university. So, I suggest that the Government should organize and invite these other students to other colleges. It should not be the parents' duty to search for the students who have not met their aggregate to go to the university.

Second. Employers. Okay, people have talked about it but I am stressing on it. The Government should lay a way of making employers to pay people according their professional qualifications not the employers given chance, just to employ the way they want, yet the make maximum use of the employee.

Third. The M.P. should have a basic education whereby basic education I mean that they should at least have ordinary level certificate and then, (I stress this). Ministers who do not have professional qualifications, people should not be appointed to be Ministers if they do not have professional qualifications – I mean maybe he reached Form IV and now, he is being appointed as a Minister for Energy, how is he going to organize that? At least, they should be professionals. Before you lead doctors, at least you must know something on medicine. So the Government should take care of that.

The Government should try to lay the issue of “one man one job”. If maybe somebody is entitled to one job, we will reduce the rate of unemployment in Kenya. You find that some people, somebody is the chairman of such and such an organization, he is being paid there, he is the Minister for what, he is being paid there, back in the village, he is something, he is being paid there while these other jobs can be redistributed to many potential Kenyans.

Com. Salim: You said “one man one job”,

Alice Sanya: Yes

Com. Salim: And the women?

Alice Sanya: By so saying a man I just don't mean this person who is walking in a trouser, even the lady.

Com. Adagala: I would like yo to state your proposal again.

Alice Sanya: One person should be entitled to one specific job – being it professional, kazi ya mkono, etc. And then, at least the Government should try to reduce the idea of forming many Commissions where they spend money and the Commissions's reports are never implemented. So, we end up wasting....

Com. Salim: What would you want done?

Alice Sanya: I would want them to stop forming many Commissions. I would suggest that they have maybe a panel or a group of people so that if there is something to be analysed on maybe teachers' salaries, we will just go to the same Commission. If there is something on Constitutional Review Commission, we will just go to that Commission. Not that we have each and every Commission for each and every problem. I think we end up wasting money. I think I have only that.

Com. Salim: Thank you Alice Sanya. Martin Owino.

Martin Owino: My names are Martin Owino. My proposals are as follows:-

On Provincial Administration. I would propose that local chiefs and assistant chiefs should be people of Form IV levels, then given relevant training like the ones given to the DOs and DCs. Then, on the DCs and the DOs, they should be posted to their local areas e.g. if someone is a Kikuyu, then he should be posted to Kikuyuland so that he can promote the social culture and norms because you find that some people are socially in different places, then if they go there, they differ with the local residents there like you don't expect a Muslim to be posted in a Christian community and he promotes the norm and the culture of those people.

Then, the other thing is when it comes to M.P.s and Cabinet Ministers. These people – we have the so called impartial defections. A situation where some MPs are not comfortable with the Parties which sponsored them to Parliament. In such like cases, I think their seats should be declared vacant so that we should go to the re-election.

Then, we have got employment security. I should propose that we should enact a law that secures the workers. Like somebody was talking about the foreign employers, let us say the private sectors. You find that there education qualifications is not being recognized. A situation where you have somebody – a qualified graduate from Kenya is being underpaid more than just a local Asian imported from India and does not know anything. So, I think a law should enacted such that you are paid as per your qualifications. Be it in private sector or in Government.

When it comes to housing, this has been a general problem especially in urban areas. I think the Government should set a body that should come and review all these houses so that they should a standard rent for specific sizes of houses.

Then, when it comes to corruption. This is mainly being promoted by the Police Force. I think the Government should set a different body that is independent (that is out of police commissioners' powers) to curb this corruption because you find that, we talk of Anti-Corruption Unit which is being headed by the Police Commissioner. It is not possible, they should have a different body to curb this corruption which is independent from Police Force.

Then, when it comes to civic education. I think this civic education body should exist regardless of being election is approaching or is not there. Because you find that when it comes to now changing of this Constitution, most of the people are ignorant. They don't know whatever that is happening. So, the civic education should continue – be it there is election or election is not there. Those are my proposals.

Com. Salim: Thank you Martin Owino. Charles Odongo, hayuko? Mary Wanjiru.

Mary Wanjiru: Mimi ningetaka kuongea upande wa Mathare North vile tuko na Shida. Jina ni Mary Wanjiru Mbugua. Sisi tuko na shida sana upande wa Mathare North, upande wa kunyakuliwa viwanda zetu ile tunaita 'parking'. Watoto wanakosa mahali ya kuchezea, hata watu wale wamekomba ma nyumba, wanakosa mahali ya ku park magari. Tuko na shida sana. Tungetaka serikali itusaidie. Vile wanaweza kutusaidia kwa sababu tumeona hakuna mahali ya ku park gari hata wale wamekomboa wameshindwa mahali ya kupitia bara barani kwa sababu huko kwote kumejengwa. Na wakikanyaga vitu ya wenyewe, wengine wanapelekwa kotini.

Com. Salim: Mama ungependelea kitu gani kifanywe?

Mary Wanjiru: Mimi ningependelea serikali ichukue hatua kali, upande ya grabbing hata kama ni koti kuchukua hatua ya kupelekwa kotini, ukweli utapatikana sababu sasa tunafanya kitu bila ukweli. Kwa sababu hata wale ma Councillor wako hapa tukienda kwao, hata hawaoni sisi kama ni watu. Ukienda kumwambia hiyo maneno, hata anawacha nyinyi hapo anaenda. Kwa hivyo tungetaka hatua tusaidiwe na serikali, vile wataweza, watusaidie mambo ya hiyo grabbing.

Ya pili, watoto wetu hapa wanashikwa. Wanashikwa, wanapelekwa Police. Wakikutwa wamesimama hapa, wanapelekwa, wanasemekana wanakunyua bangi. Kwa hivyo, tungependa tuchaguliwe wazee wa kijiji. Hawa watoto wakishikwa, tunapelekwa hapo, tunaongea mambo ya ki nyumbani halafu watoto wetu waache kwenda kutesewa huko kwa Polisi kwa sababu wanateswa sana.

Ya pili, tunataka kuchaguliwa wazee kama ishirini au thirty. Hawa wazee wanaenda kutatua mambo ya vijana, hawa wenye ma ploti. Sababu wenye ma ploti, wenyewe wenye wanalalamika sana mambo ya ma ploti, hata wenye ma ploti wanaongezewa pesa na hakuna mahali wanaenda kulalamika. Na sasa tumefika mahali ya kulalamika kwa sababu hata wale wamekomboa, wanalalamika. Pesa imeongezeka sana kutokea mwezi wa January. Watu wa World Bank hawajui hii maneno lakini watu wa City Commission wanajua hii maneno. Kwa hivyo tunaumia sana wenye ma nyumba na wale wamekomboa nao wanaumia. Kwa hivyo tunataka sana tusaidie upande wa wale wamekomboa na wenye manyumba, tusaidiane pamoja, tuone ni kitu gani kinaweza kufanyika.

Com. Adagala: Ulisema nini kuhusu World Bank?

Mary Wanjiru: World Bank? Hii pesa tumeongezewa kutokea January, watu wa World Bank hawajui lakini sisi tumeongezewa kutokea January hiyo rent, kali sana.

Com. Adagala: World Bank inaingia aje kwa rent?

Mary Wanjiru: Si tunakuta kwa kitabu imeongezwa na tunaambiwa ni World Bank wameongeza, ati uchumi iko chini. Sasa kila mtu iko na uchumi iko chini. Wale wamekomboa, uchumi yao iko chini, wenye manyumba nao wameongezwa nyumba na uchumi iko chini. Sasa tutasaidika namna gani?

Mimi nasema, wenye manyumba wanalalamika kwa wenye ma nyumba eti wanaongeza pesa na wenye ma nyumba nao wanaongezwa pesa na watu wa City Commission ati World Bank imeongeza pesa, na sasa hii loan yetu tumepewa na City Commission, sasa inaendelea tu kwenda juu tu, kwenda juu tu.

Com. Salim: Mama, wajua tatizo hilo limetajwa na wenzako hapo hawali. Sasa ungependelea jambo hili la kodi likienda juu na juu lisawazishwe namna gani?

Mary Wanjiru: Tusaidiwe. Pesa iweze kuongezwa kwa City Commission hata sisi wenye wa nyumba. Ndio nao wale wanalalamika mambo ya nyumba, wakilalamika hata serikali inasikia.

Com. Salim: Ungependa mtu gani au body gani iingilie jambo kama hili?

Mary Wanjiru: Ni Local Government kwa sababu hao ndio wameshikilia manyumba.

Com. Salim: Okay. Asante.

Mary Wanjiru: Kwa hivyo tunaomba sana kwanza turudishiwe ma parking hata wale wamekomboa ma nyumba waone mahali ya ku park magari. Asante sana.

